

## **MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MILIKI UBUNIFU DUNIANI**

**Je, wewe ni mdau, mtaalamu, au una shauku ya Miliki Ubunifu (Intellectual Property) na una malengo ya kufahamu kuhusu sekta ya Miliki Ubunifu na maendeleo endelevu nchini? Kama jibu lako ni Ndiyo, basi wito huu unakuhusu!**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Haki Miliki Tanzania (COSOTA) wameandaa Maadhimisho ya Siku ya Miliki Ubunifu Duniani yatakayofanyika tarehe 09 Mei 2024 Jijini Dar Es Salaam. Maadhimisho haya yanalenga kutoa fursa ya kutafakari kwa pamoja na wadau juu ya mahusiano yaliyopo kati ya Miliki Ubunifu (IP) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals - SDGs). Kauli Mbinu ya Maadhimisho haya ni *“Miliki Ubunifu na Malengo ya Maendeleo Endelevu: Kujenga mustakabali wa pamoja kwa kutumia ubunifu”*.

Unaweza kushiriki kama i) Mshiriki wa Kawaida ii) Mtoa Mada, iii) Kuonesha Bidhaa au Huduma katika maonesho (Exhibitor), na/au iv) Mfadhili.

### ***Jinsi ya Kushiriki***

*Ili kushiriki, tafadhali tuma maombi kwa kutumia kiungo (link) hiki*  
<https://forms.gle/XGR2TnjbYda5cMbz7>

Kwa maelezo zaidi, tafadhali tupigie kwa namba 0222212800 au tuandikie kupitia [maoni@brela.go.tz](mailto:maoni@brela.go.tz) au tembelea mitandao yetu ya kijamii ya, *Instagram: brela\_tanzania, Facebook: BRELA Tanzania, X: brela\_tanzania*

**FOMU YA USHIRIKI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MILIKI UBINIFU TANZANIA**

1. Jina:
2. Taasisi:
3. Barua Pepe:
4. Namba ya Simu:
5. Jinsia:
  - Me
  - Ke
6. Uhusika katika maonesho: *(Tafadhali andika aina ya ushiriki mf. mshiriki wa kawaida, Mzungumzaji, Muonesha bidhaa/huduma au mdhamini)*
  - Mshiriki wa kawaida
  - Mzungumzaji
  - Muonesha bidhaa/huduma
  - Mdhamini
7. Kama utapenda kushiriki kama mfadhili, tafadhali andika ni aina ya ufadhili;
  - a. Fedha taslimu
  - b. Vifaa
  - c. Nyinginezo (taja)  
.....
8. Kama majibu ya Na. 7 hapo juu ni vifaa, tafadhali taja aina ya vifaa  
.....  
.....
9. Kama ungependa kushiriki kama Mzungumzaji, tafadhali taja aina ya mada ambayo ungependa kuizungumzia (iendane na Kauli Mbiu)  
.....
10. Kama ungependa kuonesha bidhaa au ubunifu wako, tafadhali ainisha aina ya ubunifu unaotaka kuuonesha pamoja na taarifa kama ubunifu umsajiliwa kupitia hakimiliki, Hataza, alama ya biashara au huduma, nk.  
.....
11. Kama una maoni au ushauri, tafadhali andika hapa chini  
.....